**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA KILIMO**

# BODI YA PAMBA TANZANIA

# MWONGOZO NA. 1 WA MSIMU WA 2026/2027 KUHUSU MFUMO WA USIMAMIZI NA UUZAJI WA PAMBA


**Umetayarishwa na: -**
Bodi ya Pamba Tanzania,
S. L. P. 61,
**MWANZA.**

Simu : (028) 2500528.
Barua pepe : info@tcb.go.tz
Tovuti : www.tcb.go.tz


**MEI, 2026**

## UTANGULIZI

Uzalishaji na uuzaji wa pamba nchini Tanzania unasimamiwa na Sheria ya Tasnia ya Pamba Sura ya 201, marejeo ya mwaka 2023 na marekebisho ya 2025 pamoja na Kanuni za Mwaka 2011. Sheria na Kanuni zinaweka masharti ya msingi ya kuzingatiwa na mzalishaji, mnunuzi na muuzaji wa pamba ndani na nje ya nchi, pamoja na wadau wengine wa pamba. Lengo kuu la mwongozo huu ni kuhakikisha kuwa pamba inayozalishwa hapa nchini inakidhi ubora unaokubalika kimataifa ili kuiwezesha kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi. Mwongozo huu pia unalenga kumhakikishia mtumiaji wa bidhaa za pamba ya Tanzania kupata bidhaa zenye ubora wa uhakika.

Mwongozo huu unatambulika kama Mwongozo Na. 1 wa Mwaka 2026 unaohusu Mfumo wa ununuzi, usimamizi na uuzaji wa zao la Pamba ambao umeandaliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 45 ya Kanuni za Tasnia ya Pamba za Mwaka 2011 na utatumika katika maeneo yote yanayozalisha pamba nchini.

Mwongozo huu unatoa maelekezo ya jumla kwa wadau wote wa Tasnia ya Pamba nchini kuhusu utaratibu wa ununuzi wa pamba ambao utafanyika kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS). Aidha, unaweka na kufafanua utaratibu mzima wa mfumo wa ununuzi, usimamizi na uuzaji wa pamba na masharti ya msingi yaliyomo katika Sheria na Kanuni za Pamba. Utaratibu huo ni kuhusu uuzaji wa pamba, malipo kwa wakulima, usafirishaji wa pamba hadi kiwanda cha kuchambua pamba na wajibu wa kila mdau katika kutekeleza maelekezo ya Serikali kuwa wakulima wote wauze pamba yao kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi.

## SEHEMU YA KWANZA

## TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo: -

**AMCOS** Chama cha Ushirika cha Msingi kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013 na kinachojihusisha na Kilimo na Masoko.

**CCN** Hati ya kupokelea pamba viwandani.

**CDTF** Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Pamba.

**DPN** Kumbukumbu za ununuzi za kila siku (Daily Purchasing Note)

**Ghala** Jengo lililoidhinishwa kupokea na kuhifadhia pamba.

**Kituo cha Kununulia Pamba:** Sehemu iliyoidhinishwa mahsusi kwa ajili ya kuuzia na kununulia pamba kutoka kwa wakulima.

**Mnunuzi** Kampuni iliyoidhinishwa na Bodi ya Pamba Tanzania kununua na kuchambua pamba katika eneo lililoainishwa katika msimu husika.

**Kikosi Kazi cha Wilaya**: Kamati inayoundwa na Watumishi wa Serikali katika ngazi ya Wilaya kwa ajili ya ufuatiliaji na usimamizi wa mauzo ya pamba.

**Mkaguzi wa Ubora:** Mtumishi wa umma mwenye taaluma ya ubora wa pamba aliyeidhinishwa kukagua pamba iliyopo kwenye kituo cha kununulia pamba, ghala, gari, shamba, kiwanda cha kuchambua pamba na mahali pengine popote ambapo panahusika na pamba.

| | |
|---|---|
| **Sheria** | Sheria ya Tasnia ya Pamba Na. 2 ya Mwaka 2001 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2023 pamoja na marekebisho ya mwaka 2025 |
| **TCB** | Bodi ya Pamba Tanzania |
| **TGA** | Chama cha Wachambuaji wa Pamba Tanzania |
| **TCDC** | Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania. |
| **UNION** | Chama Kikuu cha Ushirika kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kinachojihusisha na Kilimo na Masoko ya mazao. |
| **WMA** | Wakala wa Vipimo |

## SEHEMU YA PILI

## USIMAMIZI WA TASNIA YA PAMBA TANZANIA

### 2.1 Sheria na Kanuni za Tasnia ya Pamba

Tasnia ya Pamba nchini inaongozwa na kusimamiwa na Sheria ya Tasnia ya Pamba Sura ya 201, marejeo ya mwaka 2023 na marekebisho ya 2025 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2011

### 2.2 Bodi ya Pamba Tanzania

Sheria ya Tasnia ya Pamba Sura ya 201, marejeo ya mwaka 2023 na marekebisho ya 2025 pamoja na Kanuni za Mwaka 2011 inaipa Bodi ya Pamba Tanzania mamlaka ya kusimamia na kuratibu shughuli zote zinazohusu maendeleo ya Tasnia ya Pamba nchini.

## SEHEMU YA TATU

## UUZAJI NA UNUNUZI WA PAMBA

3.1 Pamba yote itauzwa kupitia AMCOS ya eneo husika. Ikithibitika kuwa AMCOS iliyopo inakosa sifa kwa sababu ya ubadhirifu au uvunjaji wa sheria, taratibu na miongozo, Bodi ya Pamba inaweza kutoa kibali maalum kuruhusu kampuni kufungua kituo binafsi katika eneo hilo.

3.2 Katika kata zinazotekeleza programu ya BBT, kampuni zilizowekeza pekee ndizo zitakazoruhusiwa kununua pamba katika maeneo hayo na bei ya pamba ni lazima iwe sawa au juu ya bei iliyopo katika maeneo mengine. Kampuni itakayoshindwa kununua pamba kwa bei ya soko itaondolewa haki ya kuwa mnunuzi pekee katika kata husika. Aidha, ili kuepusha adha kwa wakulima kampuni itakayoshindwa kununua pamba kwa siku 7 mfululizo, itaondolewa sifa ya kuwa mnunuzi pekee na Bodi ya Pamba itaruhusu kampuni nyingine kununua pamba katika eneo hilo.

3.3 Kwa maeneo ambayo hayana uwekezaji, kampuni zote zitakuwa na haki ya kununua pamba baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa.

3.4 Mizani janja na ya kidijitali iliyohakikiwa na kupasishwa na Wakala wa Vipimo ndiyo pekee itakayotumika kupimia pamba ya mkulima.

3.5 Mizani janja inayotumia mfumo wa dijitali ndiyo pekee itakayotumika katika mikoa wa Simiyu, Kigoma na Katavi pamoja na wilaya za Igunga, Nzega, Kishapu, Kahama na Magu.

3.6 Malipo ya pamba ya wakulima yatafanyika kupitia njia zifuatazo;

i. Akaunti za benki au simu za mkononi. Malipo yatafanyika ndani ya saa 48 baada ya pamba ya mkulima kupokelewa kwenye kiwanda cha pamba.

ii. Fedha taslim katika kituo cha ununuzi punde uhakiki na upimaji wa pamba ya mkulima unapokamilika.

3.7 Kampuni inayonunua pamba itakabidhi fedha za kununulia pamba kwenye AMCOS ambapo ni lazima karani pamoja na wajumbe wasiopungua wawili wa AMCOS wakiri kuzipokea kwa kusaini stakabadhi ya fedha.

3.8 Kwenye fedha za gharama ya ununuzi iliyokubalika ya shilingi 60, kampuni zitalipa shilingi 57 kwa kilo katika akaunti ya AMCOS husika kwa ajili ya gharama ya ununuzi na shilingi 2 itabaki kwenye kampuni kwa ajili ya shajala na shilingi 1 itaelekezwa katika ofisi za Wakuu wa mikoa na wilaya kwa ajili ya kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa ununuzi wa pamba. Mamlaka ya uidhinishaji wa matumizi ya fedha za AMCOS itaelekeza mgawanyo wake kwa AMCOS, Vyama Vikuu vya Ushirika na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mujibu wa Waraka wa Mrajis wa Ushirika. Aidha, Bodi ya Pamba itatoa maelekezo kuhusu ukusanyaji shilingi 1 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji kwa ofisi za wakuu wa mikoa na wilaya.

3.9 Utaratibu wa ununuzi wa pamba hai (Organic Cotton) utakuwa kama ifuatavyo;

a) Kampuni itanunua pamba hai kwenye eneo ambalo Bodi ya Pamba imetoa idhini.
b) Kila kampuni inayozalisha pamba hai ni lazima iwe na ghala maalum kwa ajili ya pamba hai katika kila kijiji inakozalisha pamba hiyo. Haitaruhusiwa ghala moja kutumika kwa pamba ya kawaida na pamba hai kwa namna yoyote ile.
c) Orodha ya wakulima wa kila kampuni katika eneo husika na taarifa zao ni lazima ibandikwe katika kila ghala lililotengwa

kwa ajili ya kununulia pamba hai baada ya kuthibitishwa na Afisa Kilimo wa Bodi ya Pamba wa eneo husika;

d) Stakabadhi za mazao na nyaraka nyingine za mauzo kwa ajili ya pamba hai hazitaruhusiwa kuchanganywa na zile zinazotumika kwa pamba ya kawaida;

e) Taarifa za ununuzi wa pamba ni lazima zijazwe kwenye 'ledger' ya kampuni ambayo fomati yake itatolewa na Bodi ya Pamba, Aidha, kampuni zinazojihusisha na pamba hai na pamba ya kawaida zitakuwa na 'ledger' mbili kwa aina hizo za pamba iliyonunuliwa;

f) Ni lazima kila kampuni ibandike bango la bei yake katika ghala la kununulia pamba katika eneo linaloonekana kwa urahisi na bei hiyo ni lazima iwe juu ya bei ya pamba ya kawaida iliyoko sokoni kwa wakati huo;

g) Kumbukumbu zote za mauzo zitakuwa zinafanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara na maafisa kutoka Bodi ya Pamba kadri itakavyoonekana inafaa;

h) Kampuni isinunue pamba ya kawaida na kuitafsiri kama pamba hai.

3.10 Bodi ya Pamba itatoa leseni kwa mnunuzi kwa ajili ya kununua pamba ya wakulima kupitia AMCOS kwa kila kijiji.

3.11 Kila kampuni itakuwa na vitabu vyake vya stakabadhi ya mazao katika kila AMCOS itakayoinunulia pamba kwenye maeneo yatakayotumia mizani ya kawaida na ni lazima vijazwe kikamilifu kwa kila muamala utakaofanyika.

3.12 Kwa maeneo ambayo hayana AMCOS, kituo cha ununuzi wa pamba cha AMCOS iliyo jirani kitatumika kununulia pamba au inaweza

kufungua kituo cha ununuzi kwenye eneo husika. Hii ina lengo la kuondoa adha ya kutembea umbali mrefu kwa wakulima wakifuata sehemu ya kuuzia pamba yao.

3.13 Kila AMCOS itawajibika kuandaa taarifa ya kuonesha jumla ya kiasi cha pamba kilichonunuliwa kwa kila kampuni kwa kila siku kwa kujaza **"Daily Purchasing Note"** ya kila kampuni.

3.14 Kwa lengo la kulinda ubora na upatikanaji wa mbegu bora za kupanda kwa ajili ya msimu wa kilimo 2026/27, kampuni zitakazopewa leseni za kununua pamba katika Wilaya za Igunga na Tanganyika ni lazima zitenganishe pamba kutoka katika wilaya hizo na pamba ya maeneo mengine. Aidha, pamba itakayonunuliwa kutoka maeneo ya uzalishaji wa mbegu, itachambuliwa chini ya uangalizi wa maafisa wa Bodi ya Pamba. Ikitokea dharura njiani kama vile ajali au kuharibika kwa gari, gharama zote za ziada (kushusha, kupakia, chakula na malazi kwa msindikizaji wa AMCOS) zitalipwa na mnunuzi.

3.15 Ili kuleta ushindani katika ununuzi wa pamba kupitia Vyama vya Ushirika, wanunuzi wote walioomba kununua pamba kwenye eneo husika na kupatiwa leseni za ununuzi na Bodi ya Pamba watashiriki kwenye ununuzi kwa njia `ya ushindani kwa utaratibu ufuatao: -

i. AMCOS itanunua pamba kwa ajili ya kampuni yenye bei kubwa kuliko kampuni nyingine kwa siku hiyo. Bei hiyo ndiyo atakayolipwa mkulima.

ii. Ikiwa kampuni zote zitakuwa na bei sawa AMCOS itazinunulia kampuni kwa kufuata utaratibu wa aliyekuwa wa kwanza kuleta fedha na kuendelea. Kiasi cha pamba cha kuinunulia kampuni kitapangwa na AMCOS na kitakuwa sawa kwa kampuni zote hadi hapo bei itakapobadilika.

iii. Ni lazima mkulima apewe risiti ya kampuni iliyonunua pamba inayoonesha tarehe, uzito, bei na thamani ya pamba yote aliyouza na atalipwa kulingana na bei na thamani iliyoandikwa katika risiti.
iv. Kila mnunuzi analazimika kuwa na bango lenye kuonesha bei yake kwa kila siku katika kituo cha ununuzi ambayo haitakuwa chini ya bei dira.
v. Ili kuongeza uwazi wa bei katika vituo vya ununuzi, kila kituo cha ununuzi kitakuwa na "ledger" itakayoandaliwa na Bodi ya Pamba. Ledger hii itakuwa inajazwa na kusainiwa na Katibu Meneja wa AMCOS pamoja na mnunuzi ikionesha mabadiliko ya bei kila yanapotokea na itakuwa ikikaguliwa na mamlaka za Serikali wakati wowote ikihitajika.
vi. AMCOS itakuwa na jukumu la kukagua usafi na ubora, kupima uzito wa pamba na kuwalipa wakulima.
vii. Kabla gari halijaondoka kiwandani kufuata pamba kijijini, ni lazima lipimwe na uzito wake kujazwa katika toleo au "order" ya gari ambayo itatakiwa kuonwa na karani/katibu meneja wa AMCOS akiwa katika kituo chake cha ununuzi. Ni **LAZIMA** AMCOS ipime uzito wa kila gunia na kujaza uzito huo kwa usahihi katika hati maalum (tally sheet) kabla ya kusafirisha pamba kwenda kiwandani. Malinganisho ya awali ya uzito wa pamba yatafanyika punde gari itakapoingia katika mzani wa kiwanda na kabla ya kuishusha kwa kulinganisha uzito wa gari ulioko kwenye toleo na uzito wa pamba ulioko katika hati ya utoaji wa mazao. Ikionekana kuna tofauti isiyo ya kawaida, pamba hiyo haitashushwa na badala yake taarifa itapelekwa Bodi ya Pamba, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Wakala wa Vipimo ili kutoa uamuzi wa haki juu ya suala hilo.

3.16 Madeni ya pembejeo zilizotumika katika msimu wa kilimo wa 2025/26 hayatakatwa kutoka kwa mkulima wakati wa kuuza pamba yake.

# SEHEMU YA NNE

## WAJIBU NA MAJUKUMU YA WADAU MBALIMBALI WA TASNIA YA PAMBA

### 4.1 BODI YA PAMBA TANZANIA (TCB)

i. Kutoa leseni ya ununuzi na uchambuaji wa pamba kwa kampuni;

ii. Kutoa Mwongozo wa Serikali kuhusu ununuzi, usimamizi na uuzaji wa zao la pamba.

iii. Kusimamia, kukagua na kutoa elimu kuhusu usafi na ubora wa pamba katika ngazi zote;

iv. Kutangaza bei dira ya pamba kwa mkulima kabla ya kufungua msimu wa ununuzi;

v. Kufuatilia mwenendo wa bei ya pamba katika soko la dunia na kuratibu marejeo ya bei dira pale inapobidi.

vi. Kusimamia na kuhakikisha pamba ya wakulima iliyopelekwa viwandani bila kulipwa vituoni inalipwa ndani ya saa 48 kama ilivyoelekezwa katika kipengele cha 3.6 (i) cha mwongozo huu.

vii. Kutekeleza majukumu mengine kadri yatakavyokuwa yakijitokeza kwa kushirikiana na wadau wengine.

viii. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mwenendo wa hali ya soko la pamba duniani.

ix. Kuandaa “ledger” kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa mabadiliko ya bei na kuzisambaza kwenye AMCOS.

x. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa ununuzi wa pamba unafanyika kwa haki kwa kampuni zote zinazonunua pamba na kuchukua hatua pale itakapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa utaratibu.

## 4.2 TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA (TCDC)

i. Kutoa maelekezo ya kiwango cha gharama cha kuzingatiwa na AMCOS katika kugharamia posho ya mjumbe atakayesindikiza pamba kutoka AMCOS kwenda kiwandani pamoja na matumizi mengine ili kuepusha matumizi yasiyokuwa ya lazima;

ii. Kusimamia mwenendo mzima wa shughuli za AMCOS kwa kipindi chote cha ununuzi wa pamba ili kubaini mapungufu na kuchukua hatua stahiki mapema.

iii. Kutoa Waraka wa Mrajis ambao pamoja na mambo mengine utatoa maelekezo ya matumizi ya fedha zitakazolipwa katika AMCOS kwa ajili ya kugharamia ununuzi wa pamba.

iv. Kuhamasisha na kuhakikisha kuwa AMCOS na wakulima wote wa pamba wanafungua akaunti benki ili kurahisisha malipo.

v. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mwenendo wa hali ya soko la pamba duniani.

vi. Kusimamia na kuhakikisha pamba ya wakulima iliyopelekwa viwandani bila kufanyiwa malipo vituoni inalipwa ndani ya saa 48 kama ilivyoelekezwa katika kipengele cha 3.6 (i) cha mwongozo huu.

vii. Kusimamia na kuhakikisha kuwa fedha za kununulia pamba zinakabidhiwa kwenye AMCOS kwa karani pamoja na wajumbe wasiopungua wawili wa AMCOS kukiri kuzipokea kwa kusaini stakabadhi ya fedha.

viii. Kuhakikisha kuwa kampuni zote zilizopeleka fedha katika AMCOS zinapata pamba kulingana na fedha zilizopokelewa na fedha zilizobaki zinarejeshwa kwa wahusika.

## 4.3 TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (OR-TAMISEMI)

### 4.3.1 Ofisi ya Mkuu wa Mkoa

i. Kuratibu na kusimamia utekelezwaji wa maagizo ya Serikali likiwemo la kuhakikisha ununuzi wa pamba yote unafanyika kupitia AMCOS katika mikoa yao isipokuwa pale ambapo Bodi ya Pamba imeelekeza vinginevyo;

ii. Kupokea na kutoa mapendekezo juu ya maombi ya wanunuzi wa pamba kwa msimu husika kwa Bodi ya Pamba ili leseni za ununuzi ziweze kutolewa kwa wakati;

### 4.3.2 Ofisi ya Mkuu wa Wilaya

i. Kutoa vibali kwa wanunuzi wa pamba kulingana na maeneo yao ya uwekezaji;
ii. Kutoa vibali vya ununuzi wa pamba kwa kampuni zote zitakazokidhi vigezo katika maeneo yasiyo na uwekezaji;
iii. Kusimamia utekelezwaji wa maagizo ya Serikali likiwemo la kuhakikisha ununuzi wa pamba yote unafanyika kupitia AMCOS pekee katika maeneo yao isipokuwa pale ambapo Bodi ya Pamba imeelekeza vinginevyo;
iv. Kuhamasisha wakulima kujiunga kwenye AMCOS;
v. Kuhakikisha Kikosi Kazi cha Wilaya kinatekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa mujibu wa sheria;
vi. Kuhakikisha vikosi kazi katika ngazi ya vijiji vinaundwa na kufanya kazi zake kwa mujibu wa maelekezo ya Serikali;
vii. Kuhakikisha maombi ya wanunuzi wa pamba mbegu yaliyowasilishwa yanashughulikiwa kwa wakati;

### 4.3.3 Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri

i. Kusimamia utendaji wa AMCOS kwa mujibu wa Sheria;

ii. Kukagua na kuhakikisha kuwa kila AMCOS inajaza kwa usahihi "ledger" ya manunuzi (Daily Purchasing Note) ya kila kampuni kila siku baada ya ununuzi wa siku hiyo kukamilika.

iii. Kukagua na kuhakikisha kuwa wakulima wanaandikiwa stakabadhi kwa usahihi kwa kila muamala unaofanyika katika AMCOS. Kwa maeneo yanayotumia mizani janja, ni lazima risiti za kielektroni zitolewe kwa wakulima kwa kila muamala.

iv. Kuchukua hatua za kisheria pale inabobainika kuwa wakulima hawakupewa stakabadhi sahihi kwa pamba waliyouza.

v. Kuhakikisha kuwa kila gari inayosafirisha pamba kutoka katika AMCOS za maeneo yaliyotajwa katika kipengele cha 3.5 cha mwongozo huu inakuwa na risiti ya kielektroniki ya kutolea mzigo.

vi. Kuhamasisha maendeleo ya ushirika katika maeneo yao pamoja na ufunguzi wa akaunti za benki;

vii. Kutoa elimu kwa wakulima kuhusu mfumo wa malipo ya mauzo ya pamba kupitia akaunti zao za benki au simu za mkononi;

viii. Kuhakikisha biashara ya pamba kwenye maeneo yao inafanyika kwa kuzingatia sheria;

ix. Kusimamia na kuhakikisha kuwa AMCOS imewalipa wakulima fedha za mauzo ya pamba yao pale ambapo malipo hayo yanafanyika kwa fedha taslim.

x. Kusimamia na kuhakikisha AMCOS inawasilisha orodha ya wakulima na kiasi cha malipo yao kwa usahihi na kwa wakati pale ambapo malipo yanafanyika kupitia benki au simu ili kuwawezesha wanunuzi kulipa ndani ya saa 48 kama ilivyoelekezwa katika kipengele cha 3.6 (i) cha mwongozo huu.

xi. Kutoruhusu gari la kampuni kuchukua pamba ya AMCOS mara ya pili ikiwa deni la pamba iliyochukuliwa awali na kampuni hiyo katika AMCOS husika halijalipwa.

xii. Kusimamia ujazaji wa "ledger" ya mabadiliko ya bei kwa ajili ya ufuatiliaji wa mwenendo wa mabadiliko ya bei kwenye AMCOS.

xiii. Kuhakikisha kuwa kampuni zote zilizopeleka fedha katika AMCOS zinapata pamba kulingana na fedha zilizopokelewa na fedha zilizobaki zinarejeshwa kwa kampuni husika.

## 4.4 WAKALA WA VIPIMO

i. Kukagua na kuthibitisha mizani yote ya kupimia pamba kabla ya msimu kuanza;

ii. Kutoa mafunzo ya upimaji sahihi katika mizani kwa wakulima na AMCOS;

iii. Kufanya ukaguzi wa mizani ya kupimia pamba vituoni na viwandani wakati msimu wa ununuzi ukiendelea na

kuchukua hatua za kisheria pale inapobainika kuwa kuna ukiukwaji wa sheria;

iv. Kutatua migogoro inayotokana na malalamiko ya utofauti wa uzito wa pamba baina ya AMCOS na kampuni;

### 4.5 CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA

i. Kuandaa na kusambaza shajala zinazohitajika kwa ajili ya ununuzi wa pamba katika AMCOS.
ii. Kuratibu shughuli ya kufukiza dawa (fumigation) kwenye maghala yote yatakayotumika kununua pamba;
iii. Kuhakikisha mizani yote itakayotumika katika upimaji wa pamba ya mkulima ni ile tu iliyothibitishwa na Serikali kupitia Wakala wa Vipimo;
iv. Kuratibu utoaji wa elimu ya ushirika kwa wakulima wa pamba;
v. Kusimamia shughuli za uendeshwaji wa biashara ya zao la pamba kupitia AMCOS;
vi. Kusimamia na kuhakikisha kuwa fedha za kununulia pamba zinakabidhiwa kwenye AMCOS kwa karani pamoja na wajumbe wasiopungua wawili wa AMCOS kukiri kuzipokea kwa kusaini stakabadhi ya fedha.
vii. Kusimamia malipo ya fedha za mauzo ya pamba ya mkulima kwa kuzingatia bei halisi ya siku husika;
viii. Kuhakikisha AMCOS zote zimefungua akaunti benki zitakazotumiwa na wanunuzi kulipa fedha za gharama za ununuzi wa pamba;

ix. Kutunza kwa usahihi takwimu za ununuzi wa pamba kutoka kwa wakulima na kutoa taarifa kwa mamlaka husika zikiwemo TCB, TCDC, Halmashauri ya Wilaya ya eneo husika pamoja na wadau wengine pindi inapohitajika;

x. Kutekeleza majukumu mengine ya msingi kwa kadri yatakavyokuwa yakitolewa na TCB na TCDC.

xi. Kuhakikisha kuwa kampuni zote zilizopeleka fedha katika AMCOS zinapata pamba kulingana na fedha zilizopokelewa na fedha zilizobaki zinarejeshwa kwa wahusika.

### 4.6 VYAMA VYA USHIRIKA VYA MSINGI (AMCOS)

i. Kuajiri watendaji wenye sifa zinazohitajika katika ununuzi wa pamba na usimamizi wa fedha;

ii. Kuajiri watendaji wa kutosha kulingana na idadi ya vituo vitakavyotumika katika ununuzi wa pamba mbegu. Aidha, Bodi ya AMCOS itakuwa na jukumu la kuhakikisha kwamba pamba inayonunuliwa kutoka kwa wakulima inakuwa na ubora unaotakiwa kwa kukagua kila mzigo kabla ya kupima.

iii. Kuhakikisha kuwa maghala yote yanayotumika katika ununuzi wa pamba yamefukizwa dawa (fumigation) kikamilifu.

iv. Kuhakikisha mabango ya bei ya kununulia pamba mbegu ya kila mnunuzi yanabandikwa katika sehemu inayoonekana vizuri kwa watu wote;

v. Kuhakikisha kuwa inanunua pamba kwa ajili ya kampuni yenye bei kubwa kuliko kampuni zote kwa wakati huo na kutumia **stakabadhi ya mazao ya kampuni husika** pekee.
vi. Kupokea na kutumia vitabu vya stakabadhi ya mazao vitakavyoletwa na kila kampuni kwa ajili ya kununulia pamba katika AMCOS husika.
vii. Kukagua, kupokea, kupima na kuhifadhi pamba iliyo safi na yenye ubora iliyoletwa kwenye ghala na wakulima. Ni lazima pamba itengwe katika madaraja **"A"** na **"B";**
viii. Kuwalipa wakulima fedha zao za mauzo ya pamba katika kituo cha ununuzi baada ya kuhakikiwa na kupimwa kwa wale wanaolipwa fedha taslimu;
ix. Kutoa stakabadhi sahihi kwa kila muamala unaofanyika kwa mkulima; kwenyemaeneo yanayotumia mizani ya kidigitali inayotumia mfumo, risiti za kielektroni ndizo zitakazotumikakwa wakulima
x. Kuhakikisha kuwa kila gari inayosafirisha pamba kutoka katika AMCOS za maeneo yaliyotajwa katika kipengele cha 3.5 cha mwongozo huu inakuwa na risiti ya kielektroniki ya kutolea mzigo
xi. Kujaza kwa usahihi **"Daily Purchasing Note"** ya kila kampuni kila siku baada ya ununuzi kukamilika.
xii. Kuhakikisha kuwa kumbukumbu za jina la mkulima, bei na jumla ya fedha alizopata mkulima zinaingizwa katika stakabadhi ya mazao ya kampuni iliyouziwa pamba hiyo na mkulima husika kupewa stakabadhi yenye taarifa sahihi za mauzo yaliyofanyika.

xiii. Kushindilia katika magunia, kupima magunia, kujaza uzito wa kila gunia katika “tally sheets” na kusindikiza pamba kutoka ghala la AMCOS kwenda katika viwanda vya kuchambua pamba;

xiv. Kuandaa orodha ya malipo ya wakulima (wale wanaolipwa kupitia akaunti au simu) kulingana na kiasi cha pamba kilicholetwa na kila mkulima husika na kuiwasilisha kwa mnunuzi wa pamba hiyo kwa ajili ya malipo. Orodha ya malipo ni lazima iwe na taarifa zifuatazo;
   - Jina kamili la mkulima aliyeuza pamba;
   - Namba ya akaunti ya mkulima;
   - Namba ya simu ya mkulima iliyosajiliwa kwa jina lake;
   - Namba ya stakabadhi ya mazao aliyopewa mkulima chamani;
   - Kiasi cha kilo alizouza;
   - Bei ya kununulia pamba kwa kilo kwa siku aliyouza;
   - Thamani ya pamba aliyouza;
   - Namba ya toleo la gari pamoja na namba ya usajili ya gari iliyobeba pamba;
   - Saini ya Katibu wa AMCOS na mhuri wa AMCOS;

xv. Kufuatilia na kuhakikisha kuwa malipo ya wakulima yanafanyika mapema (ndani ya saa 48) baada ya pamba kupokelewa kiwandani;

xvi. Kutunza kwa usahihi takwimu za pamba iliyonunuliwa na kutoa taarifa sahihi kwa wadau wa usimamizi pindi zitakapohitajika;

xvii. Kuwa na akaunti benki kwa ajili ya malipo ya gharama za ununuzi wa zao na uendeshaji wa shughuli za chama;

xviii. Kuhakikisha kuwa fedha ya gharama za ununuzi itakayolipwa na kampuni inawafikia wahusika kwa mujibu wa Waraka wa Mrajis ambao utatoa maelekezo ya mgawanyo a fedha hiyo.

xix. Kupokea na kuhakikisha kuwa fedha za kununulia pamba zinakabidhiwa kwenye AMCOS kwa karani pamoja na wajumbe wasiopungua wawili wa AMCOS kukiri kuzipokea kwa kusaini stakabadhi ya fedha

xx. Kusimamia na kutekeleza majukumu mengine kwa kushirikiana na TCDC na TCB kadri yatakavyokuwa yakijitokeza;

xxi. Kutoa taarifa kwa uongozi wa kiwanda, Bodi ya Pamba na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kuhusiana na unyanyasaji, rushwa na usumbufu mwingine unaofanywa na watendaji wa mnunuzi kwa msindikizaji wa pamba wa AMCOS;

## 4.7 WAKULIMA WA PAMBA

i. Kuvuna pamba kwa kuzingatia kanuni za kilimo bora cha pamba;

ii. Kutenga pamba katika daraja **"A"** na **"B"**; kabla ya kuipeleka katika kituo cha ununuzi;

iii. Kuhakikisha kuwa anapewa stakabadhi ya mazao yenye taarifa sahihi za kiasi cha pamba aliyouza na bei aliyolipwa kwa siku husika.

iv. Kuwa na akaunti benki na kusajili simu za mkononi ili kuwezesha malipo ya pamba yao kupitia akaunti zao za benki na simu za mkononi;
v. Kutumia mifuko sahihi na inayokubalika kwa ajili ya kuvuna, kuhifadhi na kusafirisha pamba.

### 4.8 WANUNUZI WA PAMBA

i. Kuwa na leseni ya kununulia na kuchambulia pamba inayotolewa na Bodi ya Pamba.
ii. Kununua pamba kupitia AMCOS iliyopo katika eneo husika. Pamba yoyote itakayokamatwa ikiuzwa nje ya mfumo wa Ushirika itataifishwa na Serikali;
iii. Kwa kampuni zilizowekeza kupitia programu ya BBT, kuhakikisha kuwa zinanunua pamba kwa bei iliyopo sokoni kwa wakati huo. Kampuni itakayoshindwa kuendana na bei ya soko, itaondolewa haki ya kuwa mnunuzi pekee na Bodi ya Pamba itaruhusu kampuni zingine kuingia na kununua pamba katika maeneo hayo;
iv. Kuandaa na kupeleka stakabadhi za mazao, na **"Daily Purchasing Note"** ambayo muundo wake umeambatishwa na Mwongozo huu na shajala zingine kwa ajili ya kuwezesha ununuzi wa pamba katika AMCOS.
v. Kukagua na kuhakikisha kuwa **"Daily Purchasing Note"** imejazwa kila siku na kwa usahihi katika kila kituo.
vi. Kuhakikisha kuwa mabadiliko ya bei yanaandikwa kwenye risiti inayofuata baada ya risiti ya mwisho ya bei ya awali katika kitabu cha stakabadhi ya mazao pamoja na ledger

ya mabadiliko ya bei inayoandaliwa na Bodi ya Pamba. Aidha, risiti iliyoandikwa mabadiliko ya bei kuonesha tarehe na muda wa kuanza kutumika kwa bei mpya, inapaswa kubaki kwenye kitabu cha stakabadhi ya mazao ikiwa ni kumbukumbu ya mabadiliko ya bei.

vii. Kuhakikisha kwamba pamba kutoka katika AMCOS inapimwa na kushushwa ndani ya siku 2 baada ya kufikishwa kiwandani. Ikitokea ucheleweshaji wa zaidi ya masaa hayo, gharama za kujikimu za msindikizaji zitalipwa na mnunuzi kwa kiasi cha shilingi 25,000 kwa siku;

viii. Kukabidhi na kuhakikisha kuwa fedha za kununulia pamba zinapokelewa kwenye AMCOS kwa karani pamoja na wajumbe wasiopungua wawili wa AMCOS kukiri kuzipokea kwa kusaini stakabadhi ya fedha.

ix. Kulipa kwenye akaunti ya AMCOS gharama ya ununuzi ya shilingi 57 kwa kila kilo moja ya pamba itakayonunuliwa.

x. Kufanya malipo ya awali (advance payment) kwa AMCOS kupitia akaunti za AMCOS husika ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake mara tu msimu wa ununuzi unapoanza;

xi. Kulipa ushuru wa Halmashauri, Mfuko wa CDTF na Ushirika ndani ya saa 48 baada ya pamba kufika kiwandani. Kampuni haitaruhusiwa kubeba pamba kutoka kituoni kwenda kiwandani ikiwa itakuwa haijalipa ushuru wa Halmashauri na ushuru wa Ushirika kwa pamba iliyosafirishwa kabla.

xii. Kuhakikisha pamba inayopokelewa kiwandani kutoka katika maeneo yaliyotajwa kwenye kipengele cha 3.5 cha mwongozo huu inakuwa na risiti ya kielektroniki ya kutolea mzigo kutoka kwenye AMCOS

xiii. Kushughulikia kwa wakati malalamiko yote ya AMCOS kuhusiana na unyanyasaji, rushwa na usumbufu mwingine wakati wa mapokezi ya pamba kiwandani;

## SEHEMU YA TANO

## USULUHISHI WA MIGOGORO

5.1 Endapo kutatokea malalamiko ya upande mmoja kutotendewa haki na upande mwingine, mlalamikaji atatakiwa kuwasilisha malalamiko yake kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba ndani ya siku 14 tangu tarehe ya tukio.

5.2 Bodi ya Pamba itaitisha kikao cha usuluhishi ndani ya siku 21 tangu kupokea malalamiko kwa ajili ya kusikiliza na kutoa maelekezo ya namna ya kumaliza jambo husika kwa mujibu wa Sheria.

**Hitimisho:**

***Mwongozo huu unatakiwa kusomwa kwa pamoja na Sheria ya Tasnia ya Pamba Sura ya 201, marejeo ya mwaka 2023 na marekebisho ya 2025 pamoja na Kanuni za Mwaka 2011***

***Mwongozo huu umetolewa tarehe*** 12/05/2026

.....................................

***Renatus L. Luneja***

**KAIMU MKURUGENZI MKUU**